


Uchumi na BIASHARA

11 JINSI TMDA INAVYOSAIDIA KUWEZESHA UCHUMI IMARA

13 FURSA LUKUKI BANDARI NDOGO YA MKWAJA

Udhibiti uvuvi haramu na ongezeko mavuno ya samaki

Uk 12



Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki (wa pili kushoto), akiwa na aliyekuwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi na sasa ni Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo, Pauline Gekul (wa pili kulia) na Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Uvuvi) Dk Rashid Tamatamah (wa kwanza kushoto), walipozuru moja ya viwanda vya kuchakata samaki kilichopo mkoani Mwanza.

* Mifugo wataka vijana kujiunga kunufaika na mikopo *

NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Abdallah Ulega amewashauri vijana wa Jimbo la Kawe mkoani Dar es Salaam kuunda vikundi ili kufaidi fursa za mikopo zinazotolewa na wizara hiyo.

Kauli hiyo aliitoa bunge-ni jana wakati akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Kawe, Askofu Josephat Gwajima(CCM) aliyetaka kujua ni lini serikali itaanza kutoa mikopo kwa vijana wengi wanaovua kwa kutumia mitumbwi midogo katika Bahari ya Hindi.

Ulega alisema vijana wa jimbo hilo wanatakiwa

kujiunga katika vikundi ili kupata mikopo inayotolewa na wizara hiyo ikiwemo ya kununua mashine za boti za uvuvi.

“Pia wanaweza kujiunga katika vikundi ili kupata mikopo ya kutengeneza vichanja vya kukaushia samaki pamoja na kukopa mikopo kwa ajili ya kuza-lisha barafu ya kuhifadha samaki na kuwauzia vijana wengine,” alisema.

Akijibu swali jingine la Gwajima aliyechoji ni lini serikali itakuja na mpango madhubuti wa kutumia bahari kwa programu za uvuvi wa Bahari Kuu na michezo ya bahari ili

kutengeneza ajira kwa vijana wa Jimbo la Kawe hasa ikizingatiwa nusu ya jimbo hilo lipo Mwambao wa Bahari ya Hindi, Ulega alijibu, serikali inaendelea na juhudi za kuimarisha uvuvi bahari kuu.

Alisema Serikali inafufua Shirika la Uvuvi Tanzania(TAFICO) ili kuiwezesha nchi kunufaika na rasilimali za uvuvi hususan zile zilizopo katika ukanda wa uchumi wa bahari na bahari kuu.

Hadi sasa, serikali ina mpango wa kununua meli tano za uvuvi ambazo zita-vua katika maji ya kitaifa, bahari kuu, pamoja na ku-

toa leseni kwa meli kubwa zinazomilikiwa na sekta binafsi.

Serikali ina mpango wa kujenga bandari ya uvuvi katika ukanda wa Pwani ya Bahari ya Hindi, ambapo uwepo wa bandari hiyo utawezesha meli za uvuvi zinazovua katika ukanda wa uchumi wa Bahari ya Tanzania na Bahari Kuu, kutia nanga na kushusha mazao ya uvuvi.

Pia utawezesha meli hizo, kupata huduma mbalimbali zikiwemo mafuta na chakula ambapo meli hizo zitachangia kutoa ajira kwa wananchi, wakiwemo wa Jimbo la Kawe.

Wizara za Uvuvi Bara, Kilimo Z'bar zakubaliana ushirikiano

mifugo hususani mitamba ambapo wataendeleza pamoja na kutoa elimu kwa wafanyabiashara, wasafirishaji na wadau wanaohusika kusafirisha bidhaa.

**Wizara hizo
wamekubaliana
kwamba
ufuatiliaji huo
utafanyika kwa
kutumia vyombo
vya ulinzi na
usalama ili
kubaini maeneo
yenye mianya ya
uingizaji holela
wa mifugo na
mazao yake ...**

Majira Uk. 5 ,
Tarehe 08/06/2021

Kwa upande wake, Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji na Maliasili Zanzibar, Maryam Juma Saadala, alipongeza juhudi za serikali katika kukuza sekta ya mifugo nchini, kwani sekta hiyo ina mchango mkubwa katika kukuza uchumi.

Saadala alisema maazimio hayo yafanyike kwa wakati kama walivyokubaliana na kukuza sekta hiyo kwa maendeleo ya nchi.